

## Kilicho ndani ya Kasha



Kiunzi cha Adapta ya Bomba



Ufunguo aina ya Allen



Klipu za Kuelekeza Kebo
20






## 1 | **Pakua Programu ya Starlink**

Changanua msimbo wa QR ili upakue Programu ya Starlink.



setup.starlink.com




## 2 | **Tafuta Eneo la Kufunga**

Starlink yako inahitaji mwonekano wazi wa anga ili iweze kuendelea kuunganishwa na setilaiti zinaposonga juu. Vitu vinavyozuia muunganisho kati ya Starlink yako na setilaiti, kama vile tawi la mti, mlingoti, au paa, vitasababisha ukatizaji wa huduma. Tumia zana ya kizuizi iliyo kwenye Programu ili kuhakikisha umechagua eneo linalofaa la kufunga.



## 3 | **Ondoa Kiweko**

Finya kichupo cha kuachia na ukiondoe kwenye eneo lake lisilobadilika.





## 4 | **Pitisha Kebo Ndani ya Adapta ya Bomba**

Pitisha kebo ya Starlink ndani ya tundu kwenye adapta ya bomba hadi upande wa mbele.



## 5 | **Chomeka Kebo na Ufunge Adapta ya Bomba**

Chomeka kebo ndani ya Starlink yako.

Hakikisha plagi imechomekwa kikamilifu ili uso wa plagi uwe sawasawa na sehemu ya juu.

Kisha, telezesha adapta ndani hadi itoe sauti ya kidoko.



## 6 | **Funga Starlink**

Legeza skurubu na utelezeshe Adapta ya Bomba kwenye bomba lako la kufunga. Kaza skurubu kwa muda ili kuhakikisha Starlink inakaa thabiti kwenye bomba.

Unganisha ncha ya pili ya kebo ya Starlink kwenye ruta na uchomeke kwenye umeme wa ruta.



## 7 | **Fungamanisha Starlink Yako**

Arifa kwenye Programu itaonyesha ikiwa unahitaji kuzungusha Starlink ili ifungamanishwe vizuri.

Bofya arifa ili kutumia zana ya kufungamanisha.



## 8 | **Funga Ufungamanisho**

Kaza skurubu kwenye Adapta ya Bomba ili kufunga Starlink yako mahali pake.

Hakikisha Starlink yako imeunganishwa kwa uthabiti.

